# KUWABATIZA WATU KWA JINA MOJA NI FUNDISHO LA MUNGU AU LA WANADAMU???

**William Emmanuel**

Ndugu msomaji karibu tena katika jarida lingine. Leo tunaangalia kuhusu namna ya ubatizo.

Je, ni kwa majina matatu au jina moja tu?

Karibu...

Theologia mojawapo ya kipentekoste(sisemi wapentekoste wote) ni ile kwamba ubatizo lazima uwe wa kuzamisha kwa kutumia "kwa Jina la Yesu" Mdo 2:38; 8:16;10:48; 19:5; 22:16. Na sio " Kwa JIna la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu kama ilivyoelekezwa katika " Mathayo 28:19.

Mkanganyiko huu unatokana na watu wenyewe hawa kwanza hawakubali kuwepo utatu! Kwa hiyo tatizo lao la msingi sio kubatiza kwa majina matatu bali ni Utatu katika Uungu.

Hebu tuone mistari ifuatayo ambayo wanadhani inawaunga mkono katika fundisho lao;

> Matendo 2:38," ...Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo...."

Aya hiyo hapo juu; haithibitishi kuwa aliyewabatiza aliwabatiza "kwa Jina la Yesu" Jiulize mawali madogo yafuatayo;

Kwa nini Petro anawaambia wanaotaka kubatizwa badala ya kumwelekeza anayeenda kuwabatiza? Kwani walitakiwa wakajibatize au wakabatizwe? Kama walitakiwa kubatizwa, Je, ni Petro pekee ndiye aliyejua jina la kutumia wakati wa ubatizo? Kama Petro alikuwa anamaanisha wanapoenda kubatizwa wakabatizwe kwa Jina moja basi asingewaambia wao badala yake anagemwambia ambaye angewabatiza. Pili, soma tena mstari huo, utaona Petro hasemi "mkabatizwe kwa Jina la Yesu Kristo" bali Kwa Jina **LAKE** (mamlaka yake) Yesu Kristo"

> Mdo 8:16 "...Kwa maana bado hajawashukia hata mmoja wao, ila wamebatizwa tu kwa Jina lake Bwana Yesu. "
>
> Mdo 10:48 "Akaamuru wabatizwe kwa Jina lake Yesu Kristo."
>
> Mdo 19:5 " Walipoyasikia haya wakabatizwa kwa Jina la Bwana Yesu"
>
> Mdo 22:16, "Basi sasa, unakawilia nini? Simama, Ubatizwe, ukaoshe dhambi zako, ukilitia Jina lake."

Kubatizwa Jina la lake Yesu Kristo ni kubatizwa kwa mamlaka au idhini ya Yesu Kristo!

Hebu tafakari aya zifuatazo;

Mathayo 21:23-27

Katika Aya hiyo hapo juu, Wayahudi walitaka kujua Amri au Mamlaka iliyomwidhinisha Yesu kufanya shughuli ile. Sasa jaribu kulinganisha matumizi ya "Kwa Jina  Yesu" katika aya zifuatazo;

Mdo 4:8-10 "Walipowaweka katikati wakawauliza, kwa nguvu gani (utawala) na kwa Jina la nani(Mamlaka au idhini) ninyi mnafanya haya?...jueni ninyi nyote na wate wote wa Israeli kuwa kwa Jina la Yesu Kristo wa Nazareti mliyemsulubisha…..Kwa Jina hilo mtu huyu anasimama ali mzima mbele yenu…"

**Mdo 4:17-18** "Lakini neno hili (uponyaji ulio ndani ya mamlaka ya Yesu) lisije likaenea katika watu, tuwatishe **wasiseme tena na mtu awaye yote  kwa Jina hili"**

Walitakiwa kusema kwa mamlaka ya Yesu! Paulo anatukumbusha pia "na kila mfanyalo, kwa **neno** au kwa **tendo**, **fanyeni yote** kwa Jina Bwana Yesu" Wakolosai 3:17

Unawezaje kufanya kwa jina la Yesu kila neno au tendo? "Mtu akisema, na aseme kama mausia ya Mungu…" 1 Petro 4:11 ni Petro huyu huyu ndiye aliyeamriwa asiseme kwa Jina la Yesu! Katika Matendo ya mitume.

Kusema kwa Jina la Yesu ni kufanyeje? Siyo kusema kwa mamlaka ya Yesu? Tofauti yake iko wapi na kumbatizwa kwa Jina la Yesu? Je ni kubatizwa huku ukitamka Jina la Yesu? Siyo kubatizwa katika mamlaka ya Yesu? Kwa hakika ni kubatizwa katika mamlaka ya Yesu! Biblia inatukumbusha;

"Yesu akaja kwao, akasema nao, akawaambia, Nimepewa **mamlaka yote** mbinguni na duniani" Mathayo 28:18.

Mungu alimpaje hiyo mamlaka? Twasoma,

"Kwa hiyo tena Mungu alimwadhimisha mno, akamkirimia **Jina** (mamlaka) lipitalo kila jina; ili kwa **Jina la Yesu** (kwa mamlaka ya Yesu) kila goti lipigwe..." Wafilipi 2:9-11; ling. Waefeso 1:21-23; Waebrania 1:3-4.

**Mdo 5:28** "…Je, hatukuwaamuru ninyi kwa nguvu, **msifundishe kwa Jina hili**?."

Si tu waliwambia watu wabatizwe kwa Jina lake Yesu, bali pia hawa mitume walikuwa wanafundisha kwa Jina lake Yesu. Yaani walikuwa wanatekeleza agizo la Yesu! Agizo lilisemaje? –Enendeni, Mkawafanye kuwa wanafunzi wangu, mkiwabatiza, na kuwafundisha! Mathayo 28:19-20.

**Mdo 5:40** "Wakakubali maneno yake; nao walipowaita mitume, wakawapiga, wakawaamuru wasinene kwa Jina lake Yesu..."

**Mdo 8:12** “Lakini walipomwamini Filipo, akizihubiri habari njema za ufalme wa Mungu na jina lake Yesu Kristo, wakabatizwa...”

Filipo alikuwa anahubiri habari za ufalme wa Mungu na Jina lake Yesu Kristo. Alikuwa anahubirije? Je alikuwa analitamkatamka anapopita? Ni wazi kwamba, ni kukosa uelewa mpana kudhani kuwa kubatiza watu inatakiwa kutamka jina moja kwa kutumia Mdo 2:38 na 19:5 kama uthibitisho wa fundisho hili.

Katika aya zote mbili hakuna panaposema “akawatiza kwa jina la Yesu” bali “mkabatizwe kwa jina lake Yesu Kristo” na “wakabatizwa kwa Jina lake Yesu Kristo”. Kwani wakati wa kubatizwa ni nani anayetamka? Anayebatiza au anayebatizwa? Mathayo 28:18-20 ni yule anayebatiza! Sasa kama aya hizo zinathibitisha matumizi ya jina moja wakati wa kubatizwa, kwanini wanaagizwa wanoenda kubatizwa kwamba wakabatizwe kwa Jina lake Yesu Kristo badala ya kuagizwa anayeenda kuwabatiza kwamba akawabatize kwa Jina lake Yesu Kristo? Halikuwa lengo la Petro kwamba kauli ichukuliwe kama uhalali wa kutumia Jina moja wakati wa kubatiza.

Mdo 9:27-28, ”Lakini Barnaba akamtwaa, akampeleka kwa mitume, akawaeleza jinsi alimwona Bwana njiani, na ya kwamba alisema naye, na jinsi alivyohubiri kwa ushujaa katika Dameski kwa JIna la Yesu... Akahubiri kwa Jina la Bwana kwa ushujaa”

Hata kuhubiri walikuwa wanahubiri kwa jina la Yesu. Je, hapa Paulo alikuwa anahubiri kwa Jina moja?

Tumeona kwamba “Kwa Jina lake Yesu Kristo” limetumika katika Agano Jipya kudhihirisha mamlaka, madaraka au idhini na amri! Hebu ona Mdo 16:18.

Pia tumeona kwamba watu walipokuwa wanabatizwa walikuwa wanaliitia jina la Yesu (calling upon) Mdo 22:16. Yaani,walikuwa wanamwitia yeye mwenye mamlaka mbinguni na duniani. Hapo isidhaniwe kuwa waliokuwa wanabatizwa walikuwa wanaliita kwa sauti Jina la Bwana! La, bali ni kulitumaini au kuliamini Jina kwa kuziamini nguvu zake aliyemfufua katika wafu Ling. Wakolosai 2:12.

Twaona kanisa kule Korintho lilikuwa linaliitia(calling upon) jina la Bwana kama tusomavyo katika 1 Wakor. 1:2

Kwa hiyo, ni dhahiri kwamba ni makosa kubatizwa huku anayekubatiza akiwa anatamka Jina moja na kumhukumu aliyebatizwa kwa majina matatu. Yesu aliamuru watu wabatizwe kwa majina matatu; Kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu tena siyo kwa Jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu!

Yesu ndiye mwenye mamlaka, mitume aliwatuma. Kama Yesu aliagiza akisema “mkiwabatiza kwa Jina la Baba na Mwana na Roho Mtakatifu”, halafu mitume wakabatiza kwa jina moja; kwanza, wanakuwa wamekiuka taratibu waliyopewa Mathayo 28:19 na watakuwa wameshindwa kutekeleza amri ya kutufundisha walichofundishwa Mathayo 28:20.

Tunapoona mitume wamekosea (kama ni kweli) sisi haikupaswa kufanya kama walivyokosea (nasisitiza, kama kweli walibatiza kwa jina moja) badala yake sisi tungeangalia Yesu alisemaje.

Ukweli ni kwamba Mitume waliwabatiza watu kwa kufuata utaratibu aliowapa Yesu. Kundi hili linalofundisha hivi wanaelewa vibaya maneno ya Bwana Yesu juu ya Roho Mtakatifu wakisema hata ingawaje Yesu aliamuru mitume wake wakabatize kwa majina matatu, Roho Mtakatifu alipokuja aliwafundisha mitume wafanye tofauti na Yesu alivyowaelekeza. Hii ni hatari!!! Hebu tusome neno la Mungu;

“Lakini huyo Msaidizi (helper siyo assistant), huyo Roho Mtakatifu, ambaye **Baba** atampeleka **kwa Jina langu (kwa mamlaka/idhini yangu),** atawafundisha yote, na kuwakumbusha yote niliyowaambia.” Yohana 14:26

Kwenye Mathayo 28:18 Yesu aliwaambia nini mitume? Unategemea Roho Mtakatifu angewakumbusha tofauti? Kama ndivyo, basi Roho Mtakatifu ana matatizo!!! Kwa kuwa naogopa kumkufuru Roho Mtakatifu, nasema ni watu ndiyo wana matatizo ya kuelewa kilichoandikwa. Maana, twasoma;

“Lakini yeye atakapokuja, huyo Roho wa **kweli**, atawaongoza awatie kwenye kweli yote; kwa maana **hatanena kwa shauri lake mwenyewe,** lakini yote atakayoyasikia[kwa Yesu] atayanena, na mambo yajayo atawapasha habari yake. Yeye **atanitukuza mimi**, kwa kuwa atawaa katika **yaliyo yangu** na kuwapasha habari. Na yote aliyo nayo Baba ni yangu; kwa hiyo nalisema ya kwamba atatwaa katika yaliyo yangu, na kuwapasheni habari” Yohana 16:13-15

Kama ni Roho wa kweli aliidhinisha ubatizo wa Jina moja, Je, kwa nini aliamua kunena kwa shauri lake mwenye? Je ndiyo aliyoyasikia kwa Yesu? Hapa Roho huyu alikuwa anamtukuza Yesu? Lakini kazi yake kama alivyoianisha Yesu, ilikuwa ni kutwaa yaliyo katika mamlaka ya Yesu na kuwapa mitume, hata kama angechukua kwa Baba bado yote aliyo nayo Baba ni ya Yesu!

Mimi naona wazi wazi kabisa kwamba Roho mtakatifu asiingizwe mahali ambapo wametunga fundisho ili kuligawa kanisa la Kristo! Yesu aliamuru ubatizo wa majina matatu. Kama walitaka kuwa watiifu, basi walitii alichoamuru Yesu! Wakristo wa awali pia kama walitaka kuwa watiifu basi walifuata utaratibu alioamuru Yesu! Mathayo 28:18-20.